

**LESSON TRANSCRIPT****Advanced Audio Blog S1 #1****Top 10 Kenyan Holidays and Festivals:  
Concours D'Elegance**# **1**

## Tamasha la Concours D' Elegance.

Tamasha la Concours D' Elegance linahusu mashindano ya uzuri wa magari kukiwamo maonyesho ya magari ya kifahari na pikipiki. Pia mna muziki na burudani isiyo na kikomo kwa watoto. Maonyesho haya hufanyika kila mwaka, mwezi wa Septemba katika uwanja wa 'Race Course' jijini Nairobi. Tamasha hii inayondaliwa na wanaomiliki klubu ya Alfa Romeo ilianza California mwaka wa 1910 na kisha nchini Kenya baada ya miaka ishirini. Ni tamasha la kifahari zaidi na la aina yake ulimwenguni. Huonyesha uzuri na upekee iliyo katika magari ya zamani na pia iliyo kwenye bidhaa mengine ya magari ya kisasa. Wakati unaposalia, maonyesha haya yamevutia washiriki kutoka Australia, Uingereza, Ujeruman, Mauritius, Zimbabwe likiwa Afrika Kusini, Tanzania na Uganda. Tamasha hili linalojulika hasa kwa mtindo na historia unapenyeza modeli ya magari yaliyoundwa yapata miaka ya 1920. Ni katika tamasha hii pekee tunapoweza kuona magari ambayo huonyeshwa kwenya sinema pekee na ambazo hazitawezza kupatikana kwenye barabara za Kenya. Wanaomiliki baadhi ya magari haya na pikipiki hufurahia kuendesha magari yao mbele ya umati wa watazamaji walofurika uwanjani. Gari la kifahari na pikipiki hunandaliwa kwenye uwanja wa mashindano kabla ya tamasha hili la magari; hivyo basi, kuwapa fursa nzuri watu wanaotaka kuuza magari yao kwa wanoataka kununua. Tukio hili huipa Taifa la Kenya jukwaa ya kuonyesha muktadha wa kimataifa kuwa kando na kuwa na mwamba mzuri na mambuga ya wanyama pori, una uwezo wa kuandaa matukio ya msimamo wa kimataifa. Tukio hili kubwa na ambalo huchukua siku moja huisha kwa kuwatangaza washindi kwenye vikundi mbalimbali. Kuna mshindi wa jumla na washindi katika viwango vingine kulingana na miundo na wakati wa kutengenezwa. Tathmini huanza kwa kuangalia upande wa chini, ikifuatwa na jinsi nje ilivyomaliziwa, kisha upande wa ndani na hatimaye mitambo.